**JESMA 008**

# JARIBIO LA NANE K.C.P.E
# DARASA LA NANE 2021

**KISWAHILI**
**SEHEMU YA KWANZA:**
**LUGHA**

**Muda: Saa 1 dakika 40**

## SOMA KWA MAKINI MAAGIZO YAFUATAYO

1. Umepewa kijitabu hiki cha maswali na karatasi ya kujibu. Kijitabu hiki kina maswali 50.
2. Ikiwa utataka kuandika chochote ambacho si jibu andika katika kijitabu hiki.
3. Ukisha chagua jibu lako lionyeshe katika **KARATASI YA MAJIBU** na wala sio katika kijitabu hiki cha maswali.

## JINSI YA KUTUMIA KARATASI YA MAJIBU

4. Tumia penseli ya kawaida.
5. Hakikisha ya kwamba yafuatayo yameandikwa katika karatasi ya majibu:

   **NAMBA YAKO YA MTIHANI**
   **JINA LAKO**
   **JINA LA SHULE YAKO**
6. Kwa kuchora kistari katika visanduku vyenye namba zinazokuhusu, onyesha namba yako kamili ya mtihani (yaani namba ya shule. Na zile namba tatu za mtahiniwa) katika sehemu iliyotengwa mwanzo wa karatasi ya majibu.
7. Usitie alama zozote nje ya visanduku.
8. Iweke safi karatasi yako ya majibu.
9. Kwa kila swali 1 – 50 umepewa majibu manne. Majibu hayo yameonyeshwa kwa herufi A, B, C na D. Ni jibu **MOJA** tu kati ya hayo manne ambayo ni sahihi. Chagua jibu hilo.
10. Kwenye karatasi ya majibu, jibu sahihi lionyeshwe kwa kuchora kistari katika kisanduku chenye herufi uliyochagua kuwa ndilo jibu.

    **Mfano**

    **Katika kijitabu cha maswali:**

    **11.** Chagua jibu lenye nomino zilizo katika ngeli ya I - I pekee.
    A. kahawa, fedha;
    B. chumvi, chupa
    C. sukari, mvua
    D. mali, chai

    Jibu sahihi ni C

    1 [A] [B] [C] [D]   11 [A] [B] ▬ [D]   21 [A] [B] [C] [D]   31 [A] [B] [C] [D]   41 [A] [B] [C] [D]

    Katika visanduku vinavyoonyesha majibu ya swali namba 11, kisanduku chenye herufi C ndicho kilichochorwa kistari.
11. Chora kistari chako vizuri. Kistari chako kiwe cheusi na kisijitokeze nje ya kisanduku.
12. Kwa kila swali, chora kistari katika kisanduku kimoja tu kati ya visanduku vinne ulivyopewa.

**Kitabu hiki cha maswali kina kurasa 8 zilizopigwa chapa**

**Watahiniwa ni lazima wahakikishe kuwa kurasa zote za karatasi ya mtihani zimepigwa chapa sawasawa na kuwa maswali yote yamo.**

*Soma vifungu vifuatavyo. Vina nafasi 1 mpaka 15. Kwa kila nafasi umepewa majibu manne hapo. Jaza kila pengo kwa kuchagua jawabu lifaalo zaidi.*

Kijana yeyote mwenye hekima __1__ nidhamu katika mazungumzo yake. Kila mara __2__, utamsikia akiwarejelea watu waliomzidi umri kwa __3__ kama vile bwana, bibi, mheshimiwa na kadhalika. Kamwe hawezi __4__ wengine. __5__ mtu huwa mwepesi wa kuomba __6__ kwa kusema '__7__'

1. A. huzingatisha B. huzingatiwa C. huzingatishia D. huzingatia
2. A. aongeapo B. aongeaye C. aongeavyo D. aongeako
3. A. hadhi B. nahau C. nemsi D. tafsida
4. A. kuwatilia upondo B. kuwashushia hadhi C. kuwavika mbeleko D. kuwapa mkono
5. A. Akimkosea B. Anamkosea C. Angemkosea D. Alipomkosea
6. A. kusamehe B. samehewa C. msamehevu D. msamaha
7. A. hashakum B. kunradhi C. habedari D. pole

Tangu awali, __8__ kuwa mja hawezi kubadili __9__ maisha yake, hata akijitahidi vipi. Niliitilia imani hii mkazo kwa methali isemayo, "__10__". Kila nilipokosa kufanya vyema masomoni, __11__ kwamba hayo yalikuwa __12__ yangu. Mwalimu wa Kiswahili __13__ kutoka kwenye usingizi huo. Alinionya __14__ kulaza damu huku nikisingizia mapenzi ya Mola, kwamba Muumba ametupa __15__ ya kuchagua tunakotaka kuenda.

8. A. ningekuwa nimeamini B. nikiwa nimeamini C. ninakuwa nimeamini D. nilikuwa nimeamini
9. A. mwelekeo ya B. mkondo wa C. dira wa D. mustakabali ya
10. A. Jitihada haiondoi kudura B. Penye nia pana njia C. Dhamira ni dira D. Mtaka cha mvunguni sharti ainame
11. A. nilishika B. nilishikika C. nilishikizia D. nilishikilia
12. A. mapenzi B. majaliwa C. matilaba D. manufaa
13. A. Ndio alinizindua B. Ndivyo alivyonizindua C. Ndiwe aliyenizindua D. Ndiye aliyenizindua
14. A. mithili ya B. baina ya C. dhidi ya D. juu ya
15. A. hiari B. faradhi C. masharti D. dhiki

*Kuanzia nambari* **16** *mpaka* **30**, *chagua jawabu lifaalo zaidi.*

**16.** Bainisha matumizi ya kiambishi **ki** katika sentensi ifuatayo.
Mutiso aliumia mguu akicheza uwanjani kuonyesha
A. masharti
B. wakati
C. jinsi
D. mahali

**17.** Upi ni wingi wa sentensi: Hukujua kuwa angekushonea nguo kwa uzi huo.
A. Hawakujua kuwa ungewashonea nguo kwa nyuzi hiyo.
B. Hamkujua kuwa wangewashonea nguo kwa nyuzi hiyo.
C. Hamkujua kuwa mngewashonea nguo kwa nyuzi hizo.
D. Hamkujua kuwa wangewashonea nguo kwa nyuzi hizo.

**18.** Kuku ni kwa kizimba ilivyo **kasuku** kwa
A. tundu
B. kiota
C. susu
D. zeriba

**19.** Ainisha maneno yaliyoangaziwa katika sentensi ifuatayo.
Shule **hii** **ni** maridadi **kuliko** **ile**.
A. Kivumishi, kiunganishi, kielezi, kiwakilishi
B. Kivumishi, kiunganishi, kihusishi, kiwakilishi
C. Kiwakilishi, kitenzi, kihusishi, kielezi.
D. Kivumishi, kitenzi, kihusishi, kiwakilishi.

**20.** Orodha ipi inayoonyesha sauti **sighuna** pekee.
A. sh, t, p, f
B. m, ng'w, z
C. v, j, th, ny
D. s, h, n, b

**21.** Jozi ipi haijaambatanishwa ipasavyo?
A. nafasi-fursa
B. ari-ulegevu
C. doa-dosari
D. ubwede-ajizi

**22.** Akisami $\frac{5}{9}$ huandikwaje kwa maneno?
A. humusi tisa
B. humusi tano
C. tusui tano
D. tusui tisa

**23.** Tambua sentensi iliyotumia **nomino ya jamii**.
A. Kutembea huko kulimchosha sana.
B. Umati ulinisikiliza kwa makini.
C. Shangazi yake amemshauri vizuri.
D. Mafuta yale yana joto jingi.

**24.** Upi ni ukanusho sahihi wa sentensi hii?
Dola ameenda kwa daktari akapate matibabu.
A. Dola hakuenda kwa daktari akapate matibabu.
B. Dola hajaenda kwa daktari wala hajapata matibabu.
C. Dola hajaenda kwa daktari wala kupata matibabu.
D. Dola hajaenda kwa daktari akapate matibabu.

**25.** Sentensi 'Yaya alimfanya mtoto alale kitandani' ina maana sawa na
A. Yaya alimlalisha mtoto kitandani.
B. Yaya na mtoto walilala kitandani.
C. Mtoto alilazwa kitandani na yaya.
D. Mtoto alilalishwa kitandani na yaya.

**26.** Tegua kitendawili kifuatacho:
Nikitoa ninaongeza, nikiongeza ninatoa.
A. Shimo
B. Umri
C. Kula
D. Pesa

**27.** Kitu unachokidharau na kutokidhamini huenda kikawafaa wasioweza kupata kizuri zaidi.
Chagua methali inayolingana na maelezo haya.
- A. Bura yangu sibadili na rehani.
- B. Usiwatukane wakunga na uzazi ungalipo.
- C. Ganda la muwa la jana chungu kaona kivuno.
- D. Usiache mbachao kwa mswala upitao.

**28.** Chagua kinyume cha sentensi ifuatayo:
Wifi alianika nguo jua lilipochomoza.
- A. Mwamu alianika nguo jua lilipozama.
- B. Mwanyumba alianua nguo jua lilipozama.
- C. Mwamu alianua nguo jua lilipozama.
- D. Wifi alianua nguo jua lilipozama.

**29.** Kipi ni kitenzi kilichoundwa kutokana na sifa?
- A. ulegevu-legea
- B. mchovu-choka
- C. imba-mwimbaji
- D. kicheko-ucheshi

**30.** Mshororo wa pili katika ubeti wa shairi huitwaje?
- A. mloto
- B. utao
- C. mleo
- D. tathnia

*Soma makala yafuatayo kisha ujibu maswali kuanzia* **31 - 40**

Mawasiliano ni upashanaji ujumbe kutoka kwa mtu mmoja hadi mwingine. Ili mawasiliano yaafiki lengo lake, ni muhimu mambo fulani yatiliwe maanani. Baadhi ya madhara katika jamii hutokea kutokana na mushkili katika mawasiliano. Ujumbe unapowasilishwa kwa njia isiyofaa, huenda ukaleta madhara makubwa. Wataalamu wa mawasiliano hupendekeza mambo kadhaa ambayo ni muhimu katika kufanikisha mawasiliano.

Kwanza ni kujidhibiti kwa anayewasilisha ujumbe. Yeye anafaa kudhibiti hali yake hasa masolugha anayotumia. Kuna baadhi ya vitendo ambavyo huwasilisha mengi kuliko maneno yenyewe. Kasi ya kuongea na toni ya sauti ni kati ya mambo hayo. Anayewasilisha ujumbe ni muhimu akadhibiti hadhira yake au anayemsikiliza. Aidha, hana budi kudhibiti mada yake na akwepe kuzungukazunguka kabla ya kutoa kiini cha ujumbe wake. Hisia nazo zidhibitiwe na hata mandahari ya kuwasilishia ujumbe.

Vilevile, ni vizuri anayewasilisha ujumbe afanye hivyo kwa namna ya mjadala. Hali hii itamwezesha kushirikisha hadhira yake katika ujumbe pasi kuonekana kana kwamba **anahadhiri**. Asiwe anadhihirisha hisia nzito au hamaki. Mpe nafasi unayewasiliana naye ya kusema huku nawe ukimtegea sikio ndi. Hivi mawasiliano yatafanikiwa kwani yanawahusisha wote. Kamwe jizuie kuingia katika mabishano ambayo yanaweza kukuvunjia heshima.

Aidha, ni muhimu ujiamini. Hili litakupa nafasi nzuri ya kusikilizwa. Sauti yako inafaa itoke vizuri huku kasi yake ikiwa barabara na hata mkao wako uwe wa mja anayeonekana kujiamini. Sharti macho yako yalenge hadhira sawasawa. Lazima uwe na uelewa wa kutosha kuhusu kile unachozungumzia. Hilo litatokana na maandalizi yafaayo. Lau ukionyesha kusitasita na kubabaisha hadhira yako itakosa imani nawe na utaishia kutofanikiwa kuwasilisha ujumbe wako.

Umahiri katika nyanja unayozungumzia ndio huwapa watu sababu ya kukusikiliza. Huu hasa ndio unaokutofautisha na wasikilizaji wako na ikiwa kwa njia moja au nyingi[illegible] pabaya. Kwa mfano, [illegible]

unaotaka wakuunge mkono. Swali la "kwa nini nikusikilize" ni lazima ulijibu kabla ya kuikabili hadhira yako.

Utulivu ni hali muhimu katika mawasiliano. Ikiwa utaanza kwa utulivu bila shaka utaendelea na kumalizia hivyo hivyo. Jaribu udhibiti jinsi unavyopumua wakati wa kuzungumza. Tumia ishara mbalimbali za viungo vya mwili sawasawa. Matumizi ya ishara zinazoweza kueleweka vilivyo huweza kumfanya mtu kuikosea hadhira yake.

Uwazi unafaa kuzingatiwa. Kutofikia kiini cha ujumbe huifanya hadhira kupoteza makini. Usiiachie hadhira nafasi ya kukisia maana. Eleza waziwazi mawazo na malengo yako. Hivi ujumbe wako utaeleweka vyema zaidi.

Usiipotezee hadhira yako wakati. Hadhira yoyote huwa makini mwanzoni na nafasi hiyo isipotumiwa ipasavyo huenda ikapotea. Tumia maelezo mwafaka kwa muhtasari unapotoa mapendekezo, mawaidha au maelekezo. Kwa kufanya hivi, hadhira yako itakuwa katika nafasi nzuri ya kuelewa yale unayowasilisha.

---

**31.** Kulingana na aya ya kwanza,
- A. mawasiliano aghalabu huhusisha mtu mmoja.
- B. ujumbe usipowasilishwa ipasavyo huweza kuwa na athari hasi.
- C. lengo la mawasiliano hutegemea maoni ya wataalamu.
- D. mawasiliano mbalimbali huwa na lengo moja mahsusi.

**32.** Umuhimu wa masolugha ni kuwa,
- A. huonyesha ujuzi wa lugha kwa mnenaji.
- B. hupitisha ujumbe pasipohitajika mawasiliano.
- C. ni njia bora ya kuonyesha hisia za msikilizaji.
- D. huchangia kuwasilisha ujumbe katika mawasiliano.

**33.** Kuwasilisha ujumbe kwa njia ya mjadala kuna maana gani?
- A. Mpokeaji wa ujumbe ashirikishwe katika mazungumzo.
- B. Mnenaji ajaribu sana kudhibiti wasikilizaji wake.
- C. Msikilizaji apinge maneno ya msemaji ipasavyo.
- D. Ujumbe utolewe kwa njia isiyoleta migogoro.

**34.** <u>**Kuhadhiri**</u> kulingana na makala haya ni
- A. kusimulia tukio kama lilivyofanyika.
- B. kushiriki katika mjadala wa maswali na majibu.
- C. kufundisha watu au wanafunzi katika hadhara.
- D. kufanya kikao na wataalamu mbalimbali.

**35.** Ni wazi kuwa mawasiliano yanahusisha
- A. wasikilizaji na hadhira.
- B. kusema na kusikiliza.
- C. mzungumzaji na anayepitisha ujumbe.
- D. msamiati na habari.

**36.** Ni vyema kujiandaa kabla ya mawasiliano ili
- A. kupata uelewa wa mada husika.
- B. kupata kiini cha ujumbe
- C. kuelewa utakavyodhibiti hisia
- D. kuifahamu hadhira yako vizuri

**37.** Mtu huonyesha kuwa anajiamini kutokana na
- A. usikivu wake
- B. mkao wake
- C. umahiri wake
- D. msamiati wake.

**38.** Ubishi katika mawasiliano una madhara yapi kwa mujibu wa makala?

A. huwafanya watu wasiwe wasikivu.
B. huathiri kasi ya yule anayewasilisha ujumbe.
C. huweza kumshushia mtu hadhi yake.
D. huwafanya wasikilizaji kukosa imani na mnenaji.

**39.** Uwazi katika mawasiliano unahusisha,

A. kutumia ishara mbalimbali za viungo vya mwili sawasawa.
B. kuongea moja kwa moja bila kupotezea hadhira muda.
C. kudhibiti jinsi mtu anavyopumua wakati wa kuzungumza.
D. kueleza mawazo na malengo kwa njia inayoeleweka.

**40.** Ni methali gani inayoweza kutumiwa kupigia mfano kifungu kilichoangaziwa katika aya ya mwisho?

A. Nazi ni tui la kwanza
B. Mwanzo wa ngoma ni lele.
C. Mtaka unda haneni.
D. Cheche ndogo hufanya moto mkubwa.

*Soma kifungu kifuatacho kisha ujibu maswali kuanzia nambari* **41** *mpaka* **50**

Namkumbuka Kamanu tangu tukiwa katika shule ya msingi. Yamkini hakuna mwanafunzi ambaye hakumfahamu shuleni humo. Wapo waliomfahamu kutokana na unene wa mwili wake. Shule ya msingi ya Lengajuu ilikuwa ya ghorofa. Ungemtambua mara moja kwamba alikuwa akipanda vidato kwa jinsi **alivyohema**. Huenda wengine nao walimfahamu kwa kuwagota vichwa bure bilashi. Walimu walikuwa na masimulizi yao tofauti. Mwanafunzi asiyekamilisha mazoezi darasani - Kamanu. Anayevuta mkia katika mitihani si mwingine.

Kamanu hakupenda somo la kwata wala kushiriki michezo yoyote ile. Daima aliketi pembeni na kusingizia maumivu kila tulipoenda kucheza. Ajabu ni kuwa hata hakuishabikia michezo yenyewe. Alikuwa na marafiki wachache sana. Hulka yake iliwafanya wengi **wamwambae kama mkoma**.

Wakati mmoja, Kamanu aliathirika kiafya na kulazwa hospitalini kwa takriban mwezi mzima. Japo alikuwa hazidishi hapunguzi, kukosekana kwake kulitutia baadhi yetu kiwewe. Tukahofu kuwa huenda lilikuwa limemsibu jambo baya. Tulisikitika zaidi tuliposikia kwamba alikuwa amelazwa hospitalini; si wa uji si wa maji. Naikumbuka siku mwalimu wetu alipopanga tumzuru hospitalini. Kwa mara ya kwanza Kamanu alidondokwa na machozi ya furaha. Labda hakutarajia kutuona hasa akizingatia jinsi alivyotudhulumu shuleni. Lakini chambilecho wahenga, adui wako aangukapo mnyanyue.

Aliporejea shuleni baada ya kupata nafuu, Kamanu **alibadili dira ya maisha yake kabisa**. Badala ya kuzozana na wenzake, alionekana akitabasamu aliposhiriki mijadala ukariri wa mashairi na vilabu mbalimbali. Lililotushangaza zaidi ni kuona jinsi alivyoshiriki michezo kwa ari kuu. Tulianza kumfaa masomoni sasa hakung'a ng'ania kuburura mgwisho kama awali. Alikuwa katika nafasi za katikati kwenye orodha ya matokeo. "Vipi, nafasi yako ya nyuma umemwachia nani?" Tulimwuliza kiutaniutani. "Acheni hayo," alitujibu kwa tabasamu, "nafasi hiyo sikutengewa mimi."

Ilidhihirika kuwa Kamanu alikuwa na vipawa anuwai. Walimu wetu walipania kuvikuza vipawa hivi. Walimfanyisha mazoezi mbalimbali ili aimarike. Siha yake nayo ilianza kuwa mufti. Ule unene wake ukayeyuka mithili ya siagi katika kikaango. Alipenda kukimbiakimbia alipopanda vidato. Si ajabu kwamba alijitolea kutumwa majilisini hata wengine tulipolalamikia kukwea vidato vya ghorofa.

Hivi leo nimwonapo Kamanu hukumbuka kwamba hakuna kubwa lisiloshindwa. Ameinuka kuwa mmojawapo wa wanasoka watajika katika taifa hili. Ukwasi wake ni wa kupigiwa mfano.

---

**41.** Chagua jibu lililo sahihi.

A. Watu walimdunisha Kamanu kwa unene wake.

B. Mwandishi ana hakika kwamba kila mtu anamjua Kamanu.

C. Wenyeji wa Lengajuu walimfahamu Kamanu kwa sababu tofauti.

D. Msimulizi ndiye aliyefahamikiana vyema zaidi na Kamanu.

**42.** Ni wazi kwamba

A. Kamanu hakuwajibika ipasavyo darasani.

B. walimu walimchukia Kamanu kwa ulegevu wake.

C. wanafunzi wa Lengajuu walipenda kupigana shuleni.

D. walimu ndio waliosimulia mengi kuhusu Kamanu.

**43.** Wanafunzi walipoenda kushiriki michezo, Kamanu

A. alibaki darasani akijisomea.

B. alijitenga nao na kukaa pembeni.

C. alishabikia michezo pasipo kushiriki.

D. alikaa kando kutokana na maradhi.

**44.** Maneno '**wamwambae kama mkoma**' yametumia tamathali gani ya usemi?

A. sitiari

B. kinaya

C. tashihisi

D. tashbihi

**45.** Kamanu alipolazwa hospitalini,

A. wanafunzi wote waliingiwa na wasiwasi.

B. walimu waliungana kumjulia hali.

C. msimulizi ndiye aliyesikitika zaidi.

D. hakuhudhuria masomo kwa karibu mwezi mzima.

**46.** Kwa nini Kamanu alidondokwa na machozi?

A. alihofia kwamba maradhi yangemwangamiza.

B. hakutarajia kutembelewa na wale aliowadhulumu.

C. Alifurahi kumwona msimulizi na mwalimu wake.

D. hakujua maana ya methali 'adui aangukapo mnyanyue'.

**47.** Maneno '**alibadili dira ya maisha yake kabisa**' yana maana kuwa:

A. mienendo ya Kamanu, ilikuwa tofauti aliporejea.

B. maradhi yalimfanya Kamanu abadilike kimaumbile.

C. alielezwa waziwazi umuhimu wa kushirikiana.

D. ushauri wa marika ulimfanya Kamanu kubadilika.

**48.** Eleza manufaa ya michezo kwa mujibu wa kifungu

A. kujiunga na vilabu, kujua maana ya utani.

B. kuboresha matokeo, kuwaachia wengine nafasi.

C. kuimarisha afya, kumwinua mtu kiuchumi.

D. kufanikisha uhusiano, kujitenga na watu wabaya.

**49.** Kamanu kujitolea kutumwa majilisini kunaonyesha kuwa

A. amekuwa mtiifu kuliko wanafunzi wengine.

B. hapendi kuketi darasani kwa muda mrefu.

C. anajua manufaa ya elimu, si kama wengine.

D. anatamani kufanyisha mwili mazoezi.

**50.** Neno **alivyohema** kulingana na muktadha lina maana sawa na,

A. alivyochoka

B. alivyotweta

C. alivyohangaika

D. alivyolegea